

UHURU UK 8

2,115>> Megawati hizo zitaku

Ulega: Kuongeza watalii hadi milioni tano inawezekana

Na MWANDISHI WETU

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amesema lengo la serikali la kuongeza watalii hadi kufikia milioni tano ifikapo mwaka 2025, litafikiwa kutokana na ongezeko la watalii linaloonekana sasa.

Ulega alitoa kauli hiyo jana, alipotembelea baadhi ya mabanda ya washiriki wa maonyesho ya tatu ya Wiki ya Biashara na Uwekezaji mkoani Pwani, yanayofanyika Kibaha, mkoani Pwani.

Akizungumza katika banda la Wizara ya Maliasili na Utalii na banda la Halmashauri za Mafia na Mkuranga, alisema ongezeko la watalii nchini linatia matumaini.

"Inabidi tushirikiane tufanye kazi, tuwe wabunifu na kupanua wigo wa kujitangaza ili kuongeza watalii nchini na kuinua pato la taifa lifikie asilimia 30 hadi 40 na hili kwa juhudi zetu tutafika, hakuna kinachoshindikana,"



Inabidi tushirikiane tufanye kazi, tuwe wabunifu na kupanua wigo wa kujitangaza ili kuongeza watalii na kuinua pato la taifa lifikie asilimia 30 hadi 40."

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi,
Abdallah Ulega.

alisema Ulega.

Ulega alieleza hifadhi za taifa, ikiwemo Ngorongoro, Saadan, Selous na mbuga ya Vikindu Forest zinatakiwa kuongeza ufanisi, ili kuvutia watalii ndani na nje ya nchi.

Alifafanua mbuga ya Vikindu iliyopo Mkuranga ni utalii tosha, ambapo kwa sasa watalii 500 wanafika kujionea vivutio mbalimbali na wengine kwenda kupumzika kwa kipindi cha mwezi mmoja.

"Hii ni hatua nzuri ya uwekezaji endeeleni kupaendeleza ili kuongeza idadi ya watalii wa ndani na nje," alisema.

Akitembelea banda la Halmashauri ya Mkuranga, aliwataka kufanya marejesho ya tamasha la utalii katika wilaya wanayotoka ili kuleta matokeo chanya.

Akiwa katika banda la Halmashauri ya Mafia, Kaimu Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Mohammed Hussein aliwashawishi watu waende Mafia kujionea kivutio kikubwa cha Papa Potwe.

Mkurugenzi huyo alisema wavuvi wa maeneo jirani ikiwemo Zanzibar, huwa wanakwenda kumlaki samaki huyo ambaye ni kivutio.

"Samaki hawa hupatikana maeneo machache duniani na kwa mujibu wa utafiti wa bahari ni miongoni mwa viumbe vilivyopo hatarini kutoweka, moja ya maeneo wanayopatikana ni kisiwani Mafia, sehemu nyingine ni Mexico na Ufilipino," alisema.